**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

# BUNGE LA TANZANIA

## MKUTANO WA PILI

## Kikao cha Saba – Tarehe 17 Februari, 2011

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya kwa Mwaka 2009.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Udhibiti na Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, kwa Mwaka 2008/2009 [*The Annual Report and Accounts of Surface and Marine Transport Regulatory Authority for the Financial Year 2008/2009]*.

## MLIPUKO WA MABOMU
## GONGO LA MBOTO - DAR ES SALAAM

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa ridhaa yako niweze kwanza kutoa taarifa fupi kuhusiana na tukio la jana usiku ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu liweze angalau katika hatua hii kujua hali na maendeleo ya tukio la jana.

Mheshimiwa Spika, jana tarehe 16 Februari, 2011 muda wa saa 2.20 usiku ulisikika mlipuko katika moja ya Maghala ya Jeshi la Ulinzi kutoka eneo la Gongo la Mboto pale Dar es Salaam. Mlipuko huo kutoka katika ghala la tano na ni ghala ambalo linahifadhi risasi na milipuko mchanganyiko ya aina mbalimbali ikiwemo *BMW*, *Anti-tanks* na vitu vingine kama hivyo.

Taarifa ziliwafikia Wakuu kueleza kwamba kuna milipuko imesikika katika Ghala hilo. Lakini haikuchukua muda mlipuko ule ukakua, ukawa mkubwa ndani ya dakika fupi tu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mlipuko huo maghala mengine 22 pamoja na hili la kwanza yakawa 23 yote yalianza kulipuka baada ya mlipuko katika ghala lile la kwanza.

Kishindo chake kilikuwa ni kikubwa sana kwa sababu ya aina ya mabomu yaliyokuwa yamehifadhiwa humo na yameendelea kulipuka kwa kasi kubwa mpaka karibu asubuhi, alfajiri kwenye saa kumi, kumi na moja hivi ndipo iliweza kuonekana kwamba sasa kidogo hali imetuama na yalikuwa yamebaki zaidi katika ghala moja lile la 23.

Mheshimiwa Spika, kutokana na milipuko hiyo, yako mambo ambayo yamejitokeza ambayo tulizani ni vizuri mkayajua. Kwa hiyo, kwanza ni hatua ambayo Jeshi lilichukua mara tu baada ya mlipuko wa ghala la kwanza na baada ya yale maghala mengine kuwa yamelipuka na kupunguza kasi yake, walipata mpenyo sasa Viongozi wa Jeshi, kuingia katika eneo linalohusika ili kuweza kupata picha kamili ya mambo yalivyokuwa, lakini kwa ujumla maghala 22 yote yalikuwa yamekwisha haribiwa kabisa, ghala moja ndilo lilikuwa bado linaendelea kulipukalipuka na halikuwa limelipuka kwa maana ya upana kama yale mengine yaliyokuwa yametangulia.

Mheshimiwa Spika, milipuko hiyo imesababisha vilevile mabweni mawili ya wanajeshi pale na yenyewe kuharibiwa kabisa, bahati nzuri vijana waliokuwemo mule walikuwa wamepata nafasi ya kujiokoa kabla hatari haijawafikia. Lakini magari yaliyokuwepo karibu na maeneo ya maghala mawili ya *IVECO*, moja la *Refrigeration*, moja la BM 21, pamoja na *water purification* haya yote yaliharibika kabisa.

Jirani na maeneo haya kilichoweza kubainika mapema jana ni nyumba mbili ambazo zilionekana zimeathiriwa kwa kiasi kikubwa sana kwa maana ya kuteketea.

Lakini tunaamini kabisa kwa sababu ilikuwa ni usiku wa kuamkia leo asubuhi hii jitihada sasa zinazoendelea kuendelea kuainisha nyumba nyingine zaidi ambazo tunajua kwa uhakika zitakuwa zimepata madhara makubwa.

Katika milipuko hiyo moja lilikwenda likatua kwenye shule yetu ya Sekondari, lakini kwa bahati nzuri lilitua kwenye darasa na kwa hiyo, hakukuwepo na wanafunzi katika darasa lile na halikulipuka.

Mpaka leo hii asubuhi saa kumi na moja, taarifa ambazo nilikuwa nimeletewa zilionyesha kwamba kulikuwa na maiti 13 pale Amana hosipitali, maiti mbili (2) pale Temeke na Muhimbili kuna maiti mbili (2). Lakini niliarifiwa vilevile kwamba kuna fununu kwamba inawezekana zikaongezeka zaidi na tatu ndio zinaonekana za uhakika kutoka maeneo ya Kitunda kule ambako wanafuatilia asubuhi hii kupata uhakika wake.

Kwa hiyo, Jeshi lilishauri kwamba katika mazingira haya ni vizuri wananchi hasa wale ambao wako katika maeneo ya karibu ambako ndio hasa mtikisiko mkubwa

ulitokea wakawekwa kwanza mbali na eneo la tukio ili askari waweze kupata nafasi ya kupita kwenye maeneo yale na kuyaweka katika hali ya usalama zaidi. Kwa hiyo, mpaka asubuhi hii tunao wananchi karibu 4000 katika Uwanja wa Uhuru pale ambao wamehifadhiwa wakati kazi hiyo inaendelea kufanyika.

Yako mabomu vile vile ambayo yamesadikiwa yameanguka katika eneo la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa na ushauri uliotolewa jana yenyewe usiku ilikuwa ni wa aina mbili. Moja ilikuwa ni kutahadharisha ndege ambazo zilikuwa zinatarajia kutua pale jana usiku kutokufanya hivyo kwa sababu za kiusalama.

Lakini vile vile walichukua hatua nyingine kwamba uwanja ule ungefungwa kwa muda mpaka wale *field engineers* watakapopata fursa ya kuupitia na kuwa na uhakika kwamba hakuna bomu ambalo liko pale kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mriasho Kikwete, aliarifiwa jana usiku yeye mwenyewe na Mkuu wa Majeshi. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Dar es Salaam nayo ilianza kazi hiyo jana usiku yenyewe pamoja na ile ya Wilaya na Wilaya zake katika jitihada za kujaribu kuona hatua stahiki zinazoweza kuchukuliwa.

Mpaka jana usiku taarifa zilionyesha kwamba majeruhi waliokuwepo walikuwa karibu 145. Lakini asubuhi hii nimeambiwa kwamba ni dhahiri kutakuwa na ongezeko baada ya kukusanya maeneo yote ambayo jana hayakuweza kufikiwa kutokana na giza.

Jana vilevile ilionekana pengine katika hatua za haraka pengine vyombo vya habari navyo visaidie kuanza kutoa taarifa ya tahadhari kwa ajili ya wananchi ili waweze angalau kuchukua tahadhari kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

Kwa hiyo, redio zilitumika lakini na Televisheni vilevile zilitumika. Wamewasisitiza wananchi wasisogee kwenye maeneo yale ya tukio na wakiona jambo lolote ambalo linaoneka si la kawaida kwa maana ya kitu ambacho unakiona ni kipya katika mazingira yako basi wameomba sana watoe taarifa mapema kwenye Vituo vya Polisi au Jeshi ili waweze kujiridhisha na ni kitu gani hicho.

Lakini vile vile wameomba sana hata kama watagundua wasishike kitu chochote ambacho wanahisi kinaweza kuwa ni bomu badala yake watoe taarifa. Mambo mawili ambayo tunayatarajia leo. Kwanza Rais ameitisha kikao cha dharura cha Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa ambalo litakutana. Hivyo baadhi ya Mawaziri hapa wameshaondoka, Waziri na Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ameshaondoka, lakini tumemwomba Waziri wa Fedha, pamoja na Waziri wa Mambo ya Ndani nao vilevile waende.

Lakini vilevile kama ilivyo desturi Jeshi nalo itabidi waunde Baraza la Kuchunguza kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taifa ili kuweza kutafakari na kubaini hasa chanzo ni nini na hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Kwa hiyo, mwisho nataka niwape pole sana wale wote ambao wamepatwa na tatizo hili lakini kwa namna ya pekee kabisa tunatoa rambirambi za dhati kwa niaba ya Serikali, kwa Watanzania wote, kwa familia na jamii ambazo zitakuwa zimepoteza ndugu zao kutokana na mtikisiko huu ulitokea jana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana. Kutokana na hali ilivyo ya kutokea usiku huu, tena kuamkia mpaka asubuhi hii Watanzania wengi wamewekwa katika hali ya wasiwasi wengine hawafahamu kama ndugu zao wana hali gani, na mazingira yote mnaona ni ya kutisha sana.

Kwa hiyo, nitaahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

Sasa kabla ya kufanya hivyo naomba Kamati zifuatazo waende kwenye vyumba husika. Kamati ya Fedha na Uchumi waende *CDA*, Kamati ya Miundombinu waende Ukumbi wa Msekwa B, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) waende *St. Gasper Hotel*, Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma (POAC) waende *LAPF*, Kamati ya Sheria Ndogo waende Chumba Namba 133, Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama waende Chumba Namba 227.

Aidha Kamati ya Huduma za Jamii, waende *St. Gasper Hotel*. Kamati ya Maendeleo ya Jamii, nao waende *Dodoma Hotel*. Kamati ya Ardhi Maliasili na Mazingira waende *Dodoma Hotel,* Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, waende Ukumbi wa Pius Msekwa A, wakati Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC),* waende *Basement*.

Kamati ya Viwanda na Biashara, waende Chumba Namba 219. Kamati ya Nishati na Madini, waende Chumba Namba 231 wakati Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala waende *Basement*.

Waheshimiwa Wabunge tumeamua hivyo kwa sababu nchi imekaa katika mrindimo wa masikitiko, mrindimo wa wasiwasi kwa hiyo sisi hatuwezi kuendelea kufanya kazi hii. Kwa hiyo, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. Asante sana.

*(Saa 3.15 Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 18 Februari, 2011 Saa Tatu Asubuhi)*